# BUDGET HIGHLIGHTS

MWONGOZO WA WANANCHI

2012/13



Juni 2012

## KUENDELEZA UWEKEZAJI KWENYE MUUNDO MSINGI ILI KUHAMASISHA UKUAJI

- Shilingi bilioni 123.6 zimezotengewa uboreshaji wa Barabara za mijini na vijijini, ikiwa ni ongezeko la 18.5% kutoka Shilingi bilioni 104.3 ya bajeti ya mwaka wa 2011/12. Hii ni pamoja na Shilingi bilioni 2.0 za mradi wa LAPSSET;
- Shilingi bilioni 79.9 zimetengewa Kawi, fedha hizo zikiwakilisha ongezeko la 40 % kutoka shilingi bilioni 57.5 za bajeti ya mwaka wa 2011/12;
- Shilingi bilioni 1.5 zimetengewa Mfumo wa Usafiri wa Reli katika Miji ili kuhakikisha kukamilika kwa Reli inayounganisha JKIA mpaka Kituo Kikuu cha Reli katika mwaka wa 2012/13;
- Shilingi bilioni 18.8 zimetengewa sekta ndogo ya Usafiri ;
- Shilingi bilioni 8.0 za ziada za upanuzi na ujenzi wa muundo-msingi wa unyunyiizia ji wa maji katika sehemu zote nchini;
- Shilingi 7.2 bilioni zimetengewa sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT).




Barabara Mpya ya Thika Super highway, sehemu ya Ruaraka-Roasters

## UJENZI WA TAIFA BORA – KUTHIBITI MAENDELEO YA KIUCHUMI NA KIJAMII

- Ukuaji wa Kiuchumi wa 5.2% unatazamiwa katika mwaka wa 2012, ukitarajiwa kufikia kiwango cha 5.6 % katika mwaka wa 2013 na 6.0% katika mipango miaka michache ijayo. Katika kipindi cha 2012/13, hali hii inaashiria ukuaji wa kiwango cha wastani cha 5.5%;
- Mfumko wa bei ulifikia 14.0% katika mwaka wa 2011, lakini unatarajiwa kushika hadi 9.0% katika mwaka wa 2012 na baada ya hapo kufikia kiwango cha 5% kwenye kipindi cha miaka michache ijayo;
- Nakisi ya Bajeti ya 6.5 % katika Jumla ya Mapato ya Bidhaa (GDP) inatazamiwa kwenye mwaka wa 2012/13, huku ikitazamiwa kupungua zaidi hadi 3.5% kufikia 2014/15 ;
- Ugavi wa Deni la Umma kutoka kwa Jumla ya Mapato ya Bidhaa unatazamiwa kupungua kutoka 45.5% kufikia mwisho wa mwezi wa Juni, 2012 hadi 42% kufikia mwaka wa 2014/15;
- Shilingi Milioni [490mn] za Mradi wa Kimaendeleo wa Vijana wa Kenya (Kenya Youth Empowerment Project (KYEP) zitasimamia malipo ya kazi za ujima, ukuzaji wa maarifa na miradi ya mafunzo kazini ili kuwawezesha vijana kuwa na maarifa ya kutosha ya kupata ajira;
- Shilingi bilioni 233.1 zimetengewa sekta ya Elimu, zikihusisha kutoka shule za chekechea, msingi upili na Elimu ya vyuo na kadhalika utendakazi na usimamizi wake; hii ikiwa ni ongezeko la 9.2% ukilinganisha na Shilingi bilioni 213.3 zilizokuwa zimetengewa bajeti ya mwaka wa 2011/12;
- Shilingi bilioni 85.0 zimetengewa sekta ya afya, ikiwa ni ongezeko la 16.7% ukilinganisha na bilioni 72.8 zilizokuwa zimetengewa bajeti ya mwaka wa 2011/12;
- Shilingi bilioni 9.6 zimetengewa mitandao ya Usalama wa Kijamii ili kuwakinga wananchi walio maskini na wachochole kwenye jamii zetu; na
- Shilingi bilioni 1 .0 iliongezewa kwa ajili ya Hazina ya Kilimo-Biashara ili kuimarisha upatikanaji wa mikopo kwa kufanikisha kilimo cha kisasa.

## MTAZAMO WA BAJETI




| MACROECONOMIC OUTLOOK, 2011/12 - 2014/15 | 2010/11 Est. | 2011/12 Prov. | 2012/13 Proj. | 2013/14 Proj. | 2014/15 Proj. |
|---|---|---|---|---|---|
| Real GDP growth | 5.0% | 4.8% | 5.5% | 5.9% | 6.4% |
| Investment (% of GDP) | 21.3% | 22.6% | 23.6% | 24.4% | 24.8% |
| Gross National Savings (% of GDP) | 10.6% | 11.5% | 14.9% | 17.1% | 19.2% |
| Exports of goods & Services (% of GDP) | 28.4% | 26.9% | 24.9% | 24.7% | 0.0% |
| Imports of goods & Services (% of GDP) | 43.4% | 43.2% | 37.8% | 35.9% | 0.0% |
| Nominal GDP growth | 12.8% | 18.8% | 17.3% | 13.3% | 12.2% |
| Real GDP per capita growth | 2.5% | 2.8% | 3.4% | 3.6% | 3.9% |
| GDP deflator | 7.3% | 13.4% | 11.3% | 7.1% | 6.4% |
| CPI Index (avg) | 6.9% | 16.0% | 9.8% | 6.3% | 5.0% |
| Current account (% of GDP) | -10.8% | -11.1% | -8.7% | -7.3% | -6.1% |
| Revenue (incl. AiA) | 667.5 | 804.3 | 955.5 | 1,092.0 | 1,233 |
| *% of GDP* | *24.1%* | *24.4%* | *24.7%* | *24.9%* | 25.6% |
| Expenditure | 811.9 | 1,082.8 | 1,263.1 | 1,307.1 | 1,461 |
| *% of GDP* | *29.3%* | *32.9%* | *32.7%* | *29.8%* | 30.4% |
| Budget Deficit(inl.grants) | (125.9) | (228.3) | (249.4) | (166.6) | (172) |
| *% of GDP* | *-4.5%* | *-6.9%* | *-6.5%* | *-3.8%* | -3.6% |
| Public Debt (net) (KSh billion) | 1,353 | 1,525 | 1,828 | 1,846 | 2,110 |
| GDP (in KSh billion) | 2,773 | 3,295 | 3,866 | 4,383 | 4,813 |

| GOVERNMENT EXPENDITURE BY SECTOR, 2010/11 - 2012/13 | 2010/11 Est. | 2011/12 Proj. | 2012/13 Proj. |
|---|---|---|---|
| Agriculture and Rural Development | 38,197 | 52,955 | 53,257 |
| Physical Infrastructure | 165,811 | 219,002 | 267,293 |
| General Econ.Comm. & Labour (GECLA) | 12,296 | 19,469 | 21,827 |
| Governance, Justice, Law, and Order | 98,738 | 106,133 | 132,431 |
| Education | 201,750 | 213,877 | 232,362 |
| Health | 57,377 | 72,751 | 85,029 |
| Social Protection, Culture &Recreation | 34,170 | 38,091 | 38,023 |
| Public Administration and International Relations | 89,176 | 110,531 | 138,979 |
| National Security | 50,394 | 78,560 | 83,454 |
| Environmental Protection, Water and Housing | 47,418 | 47,707 | 55,206 |
| Total | 795,327 | 959,075 | 1,107,863 |

***Expenditure exclude CFS***

### Mapendekezo ya Ushuru

- Ushuru wa nyaya za kulehemu umependishwa kutoka 0% hadi 10%;
- Ushuru wa Runinga za Dijitali na zana-tepe za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Teknohama) umeondolewa;
- Ushuru wa Vyambolishe (vyakula m'badala)umepunguzwa kutoka 10% hadi 0%;
- Utoaji wa Ushuru kwa watengenezajiwa wa Vyambolishe (vyakula m'badala) kwa matumizi wa watoto wachanga na PLWH;
- Kubatilishwa kwa Ushuru wa Wana-Maduhuli wanaoleta bidhaa za Ufugaji wa Nyuki .
- Mapato ya Wamiliki wa nyumba kutozwa ushuru;
- Kila Mfanyikazi wa Kitaifa atalazimika kulipa ushuru
- Mswada Mpya wa Ushuru wa Mapato utarahisisha na kuimarisha shughuli ya utozaji ushuru na
- Mipango mingine mingi ya kiusimamizi .

## RASILIMALI ZA KUTOSHA ZITATENGEWA MIRADI YA UNYUNYIZAJI WA MAJI ILI KUSHUGHULIKIA KIKAMILIFU SWALA LA UHABA WA CHAKULA KATIKA MAENEO YOTE NCHINI

Serikali imetoa rasilimali za ziada ili kuisaidia miradi iliyokuwa imeanzishwa mwaka wa 2011/12 kwa lengo la kufufua shughuli za kilimo kupitia kwa unyunyizaji wa maji na hali kadhalika kuhakikisha kwamba tatizo la uhaba wa chakula nchini linamalizika kabisa. Shilingi bilioni 8.0 zimetengewa Hal-mashauri ya Kitaifa ya Unyunyiziaji Maji (NIB) ili kumalizia miradi yote ya unyunyiziaji maji iliyokuwa imeanzishwa katika mwaka wa 2011/12 na kuanzisha miradi mingine katika sehemu zote nchini.

Ufanisi wa miradi hiyo unaonyesha kwamba kuna miradi 4 ya wadau wadogo iliyo katika eneo la ujumla wa ekari 753 ambayo imekamilika. Miradi ya Unyunyiziaji maji ya 'Katilu Irrigation Scheme katika Kaunti ya Turkana (ekari 1,200 za mahindi), Bura Irrigation Scheme ( ekari 7,000 za mahindi), Ahero na Kano Magharibi (ekari 6,000 za mchele) kati ya nyingine nyingi. Kaunti za Turkana na Kajiado, pamoja na Kitui kwa sasa zitachangia pakubwa katika hifadhi ya chakula cha kitaifa wakati ambapo miradi yote hii itakapoanzishwa kikamilifu.

Matokeo mazuri pia yameelezewa kuhusiana na miradi mingine ya kilimo kama vile ule wa; Kibwezi (Kaunti ya Ma-kueni), Birikani (Kaunti ya Kajiado), Mitinguu na Muringa ( Kaunti ya Meru),Wikithuki (Kaunti ya Kitui), Rapsu (Kaunti ya Isiolo), Githiru (Kaunti ya Murang'a) na Maira Makemo ( Kaunti ya Busia)

## MIRADI YA UNYUNYIZAJI WA MAJI



Bura (ekari 7,000 za mahindi) - Januari 2012



West Kano (ekari 3,000 za mahindi)--Desemba 2012

**Mradi wa Katilu Irrigation Schemes huko katika kaunti ya Turkana ( Mahindi**



**Mahindi yaliyokomaa katika mradi wa Katilu Irrigation SchemeScheme— Picha NIBPicha iliyopigwa Novemba 2011. Na NIB**

Mgao huo wa shilingi bilioni 8 kwa sekta ya kilimo utahakikisha uendelevu na kudumu kwa miradi hii ya unyunyiziaji mashamba maji na hali kadhalika kuanzisha miradi mingine mipya katika maeneo yote nchini. Ili kushughulikia la kutopatikana Kilimokutopatikana kwa mikopo, Hazina ya Kilimo--Biashara imeongezewa kitita cha shilingi bilioni 1 katika bajeti ya 2012/13. Maagano haya pamoja na mikataba na benki za kuwekeza shilingi 10 kwa kila shilingi ya serikali ikiwekezwa ili kujikinga na mazingira ya athari. Uwekezaji huu utafanya usawa Kilimousawa wa kimapato katika benki za kibiashara kwa lengo la kuwekeza katika Hazina ya Kilimo--Biashara hadi shilingi bilioni 10. Uwekezaji huu unatazamiwa kuimarisha Kilimo na kukifanya kuwa biashara nzuri na kuwavutia wawekezaji wa kibinafsi wa vijana.



**Mhe. Charity Ngilu, Waziri wa Maji na Unyunyizaji, akimhoji mkulima wa unyunyiziaji mimea maji huko Birikani, Kajiado, 31 Januari, 2012**

## UTENDAKLAZI NA AJIRA KWA VIJANA

Ili kuongeza nafasi za kazi kwa vijana wetu, Serikali itatumia Shilingi milioni [491] katika Mradi wa Kuwawezesha Vijana wa Kenya, zikihusisha malipo ya kazi za ujima na Huduma nyingine kwa jamii. Fedha hizo pia zitasaidia katika mafunzo ili kuwapatia vijana wetu maarifa mahususi yanayofaa.

Mashirika ya Sekta ya Kibinafsi yanaombwa kuchukua fursa hii ili kutoa nafasi za kazi katika mafunzo ya kikazi kwa vijana. Afisi ya Uwezeshaji wa Miradi hii itabakia kuwa ile ya Waziri Mkuu, Wizara ya Maswala ya Vijana, na Wizara nyingine husika, huku KEPSA ikiwa ndio mshirikishi mkuu wa uhusika wa mashirika ya kibinafsi. Serikali pia imeboresha Hazina ya Maendeleo ya Vijana kwa kuwatengea shilingi milioni 550 na Hazina ya Maendeleo ya Wanawake kutengewa shilingi milioni 400 ili kuendelea kutoa mtaji wa kutosha kwa vijana na wanawake kwa lengo la kuwawezesha kuanzisha biashara na mipango yao ya uwekezaji.



Chuo-Anuwai kimepewa zana za kufanyia biashara

## MIPANGO YA MATUMIZI YA 2012/13

- Shilingi bilioni 171.8 za Elimu ikiwa ni pamoja na Elimu ya shule za msingi na upili na pia mishahara ya walimu
- Shilingi bilioni 85.0 za Huduma za Afya za kukinga na kutibu
- Shilingi bilioni 9.6 za mitandao ya usalama kwa jamii
- Shilingi bilioni 123.6 za barabara
- Shilingi bilioni 79.9 za Kawi
- Shilingi bilioni 53.3 za kilimo
- Shilingi bilioni 49.2 za mazingira, maji na unyunyiziaji-maji
- Shilingi bilioni 8.0 kwa unyunyiziaji-maji
- Shilingi bilioni 15.4 za Mabadiliko ya mahakama
- Shilingi bilioni 17.0 za Mabadiliko ya Bunge
- Shilingi bilioni 65.9 za Usimamizi wa Wilaya na Usalama wa Ndani
- Shilingi bilioni 14.9 za Huduma za Magereza
- Shilingi bilioni 83.5 kwa Jeshi na Huduma za Ujasusi katika Usalama wa Kitaifa
- Shilingi bilioni 17.5 za IEBC na shughuli za Uchaguzi Mkuu;
- Shilingi bilioni 1.5 za Mipango ya Hifadhi ya Nafaka (SGR);
- Shilingi bilioni 2.0 za Misaada ya Athari ya Ukame;
- Shilingi bilioni 5.0 za Hazima ya Dharura ili kushughulikia matumizi ya maswala-ibuka


## USAFIRI WA RELI MIJINI– UPUNGUZAJI WA GHARAMA ZA USAFIRI JIJINI NAIROBI

Wakazi wa jiji la Nairobi hivi karibuni watafurahia usafiri bora na wa gharama nafuu. Shilingi bilioni 1.45 zimetengewa mfumo wa Usafiri wa Reli wa Kisasa kabisa ili kuunganisha reli inayounganisha Uwanja wa Ndege (JKIA) na Kituo Kikuu cha Reli katika mwaka wa 2012/13.



**Mhe. Amos Kimunya alipokuwa akizindua Kituo Kipya cha Huduma ya Usafiri wa Reli jijini Nairobi - huko Syokimau-**

## NI FEDHA NGAPI ZITATUMIKA ?




*Fahamu: Mgao kama asilimia ya Matumiziya Jumla ya Wizara yaliyotengwa*

## KUENDELEA KUWAJIBIKIA UTEKELEZWAJI WA KATIBA

- Shilingi bilioni 15.4 za Mahakama ili kuendeleza marekebisho na mifumo mingine muhimu ya utekelezwaji wa majukumu ya Kikatiba; ikiwa ni pamoja na kushughulikia kesi nyingi zilizopo za kibiashara;
- Shilingi bilioni 17.0 za Bunge la Kitaifa ikihusisha kuunda mifumo inayofaa ikiwa ni pamoja na kuzindua Majukumu kamili ya Bunge la Kaunti baada ya uchaguzi mkuu ujao;
- Ongezeko la shilingi bilioni 17.5 za IEBC kwa lengo la kushughulikia Uchaguzi Mkuu wa 2012/13;
- Shilingi bilioni 83.5 kwa Ulinzi na Shirika la Kitaifa la Ujasusi ili kushughulikia vitisho vya kiusalama wa taifa kikamilifu na hali kadhalika kushughulikia miradi ya usasaishaji wa mambo;
- Shilingi bilioni 65.9 za kuimarisha utendakazi wa Usalama wa Ndani;
- Shilingi bilioni 5.5 za Hazima ya Usawa wa Migao

## KUWALINDA MASKINI NA WASIOJIWEZA - MITANDAO YA USALAMA WA KIJAMII

Shilingi bilioni 9.6 zimetengewa mitandao ya usalama wa kijamii ili kuwalinda wananchi maskini na wasiojiweza katika jamii zetu Hususan:

- Shilingi bilioni 4.4 zimetengewa mayatima na watoto wanaotoka katika jamii ya wasiojiweza;
- Shilingi milioni 342 za kushughulikia miradi ya fedha zitakazowasaidia walemavu;
- Shilingi bilioni 1.0 zitatumiwa kuwashughlikia wazee, huku kila mzee akipata shilingi 2,000 kwa Mwezi ;
- Shilingi bilioni 2.1 zimetengewa mradi wa kuwalisha chakula watoto shuleni- zikishughulikia shule zilizo katika maeneo kame nchini ;
- Shilingi bilioni 2.0 za miradi ya Usaidizi katika maeneo kame ;
- Shilingi milioni 925 kwa miradi ya kuwafaa watu maskini wanaoishi mijini ;
- Shilingi milioni 178 ili kushughulikia Usaidizi wa Chakula katika Maeneo ya Miji ( mifuko ya kubebea nafaka );
- Shilingi bilioni 1.04 zimetengewa kuwashughulikia mayatima werevu na watoto kutoka kwa jamii maskini katika shule za upili kwenye sehemu zote nchini.
- Shilingi milioni 300 zimetengewa ununuaji wa sodo/milembe ama ufyambo kwa ajili ya wasichana; na
- Ili kuondoa kabisa swala la kuwepo kwa kambi za wakimbizi wa Baada ya Uchaguzi na Maeneo ya vyanzo vya maji ya msitu wa Mau, Serikali imetenga shilingi bilioni 1.8 na hivyo basi kufikisha gharama yote ya shughuli hiyo ya kuwahamisha wakimbizi wa baada ya uchaguzi kuwa shilingi bilioni 15.0 kutoka mwaka wa 2008.

### Mukhtasari wa Mitandao ya Usalama wa Kijamii (Ksh. Mn)

| SAFETY NETS | 2011/12 | 2012/13 |
|---|---|---|
| National Council for Persons with Disabilities | 302 | 342 |
| Orphans and Vulnerable Children | 2,842 | 4,404 |
| Cash transfer to urban poor | 845 | 845 |
| Cash transfer to to persons with severe disabilities | | 385 |
| Food subsidy to urban poor | 198 | 178 |
| Resstlement of IDPs | 4,157 | 1,800 |
| Street Children Rehabilitation Fund | 100 | 100 |
| Girl Child(sanitary towels) | 300 | 300 |
| Older Persons Cash Transfer | 1,000 | 1,000 |

## VIPASHO VYA BAJETI YA 2012/13

### MATUMIZI YANAYOLINGANIA MASKINI

- Shilingi bilioni 8.3 kwa Elimu ya bure ya shule za msingi
- Shilingi bilioni 19.7 kwa Elimu ya bure ya shule za Upili
- Shilingi bilioni 40.8 kwa Huduma za Afya (Ukingaji)
- Shilingi bilioni 44.2 kwa Huduma za Afya (Uponyaji)
- Shilingi bilioni 118.7 kwa Mishahara ya Walimu
- Shilingi milioni 400 kwa miradi ya kazi za umma za ujima ili kushughulikia maswala ya ajira ya vijana
- Shilingi bilioni 9.6 kwa miradi ya mitandao ya Usalama wa Kijamii

### KUJIWEKA TAYARI KWA UGATUZI

- Gharama za Shughuli na Mipango ya Ugatuzi inakisiwa kuwa Shilingi bilioni 148.0 . Rasilimali zimetengwa ili kushughulikia majukumu hayo katika ngazi ya Kitaifa, kabla ya kushughulikia ngazi ya kazi pindi Serikali za Kaunti zitakapoanzishwa baada ya Uchaguzi Mkuu ujao.
- Shilingi bilioni 5.5 kwa Hazina ya Usawa wa Mgao ukiwa ni mgao wa mwaka wa 2011/12 na 2012/13 ; ikiwa shilingi bilioni 2.5 tayari zimetengewa ili kutoa Huduma za kimsingi kama vile; maji, barabara, umeme hasa katika maeneo yaliyotengwa; ; na salio la shilingi bilioni 3.0 zimewekwa pembeni zikisubiri vigezo vya kuelekeza maeneo yaliyotengwa kwa lengo la kuendelezwa na CRA; na
- Shilingi bilioni 21.2 zimetengewa Hazina ya Maeneo Bunge (CDF).

### MATUMIZI YA MAENDELEO

- Shilingi bilioni 123.6 kwa Sekta ya Barabara
- Shilingi bilioni 79.9 kwa Sekta ya Kawi
- Shilingi bilioni 8.0 kwa Upanuzi na Ujenzi wa Miradi ya Unyunyiziaji Maji nchini kwote
- Shilingi bilioni 53.3 kwa Huduma za Kilimo na Shilingi bilioni 1.0 kwa Hazina ya Kilimo-Biashara
- Shilingi bilioni 1.5 kwa Ujenzi wa Reli ya Abiria jijini Nairobi na viungani mwake

## KUWEKEZA KATIKA ELIMU



Uwezo wa maendeleo ya nchi yetu unawategemea pakubwa wananchi wenyewe. Wafanyikazi bora ndio kiungo muhimu katika kuyafikia malengo na maazimio yetu. Changamoto iliyopo kwa sasa, ni jinsi ya kufikia kiwango kinachohitajika cha wafanyikazi bora na wenye utaalamu wa kutosha katika mabadiliko tunayoazimia na kuwa na uchumi anuwai. Bajeti ya mwaka wa 2012/13 inaendelea kuwekeza pakubwa katika Elimu na hali kadhalika kuwekeza kwenye mbinu muafaka za kuwasaidia watu wasiojiweza katika jamii kwa kupitia mitandao ya usalama wa kijamii.

Serikali imetenga shilingi bilioni 8.3 ili kushughulikia Elimu ya bure ya shule za msingi na shilingi bilioni 118.7 ili kushughulikia mishahara ya walimu, ikiwa ni pamoja na kuwaajiri walimu 10,000 zaidi katika mwaka wa 2012/13. Shilingi bilioni 19.7 zimetengewa ili kusimamia gharama ya mafunzo katika shule za Upili huku shilingi bilioni 1.9 zikitengewa ujenzi wa madarasa na kuboresha muundombinu katika shule za msingi na zile za upili.

Shilingi bilioni 1.04 zimetengewa kwa misaada ya Karo za shule na ufadhili wa masomo kwa watoto werevu wanaotoka kwenye jamii maskini , huku shilingi milioni 300 zikitengewa kwa ajili ya ununuaji wa sodo ama ufyambo kwa wasichana.




# FAHAMU JINSI USHURU WAKO UNAVYOTUMIKA

## MAENDELEO KWA WOTE

Maendeleo yenye Usawa katika majanibu ya maeneo yenye umaskini mwingi yataboreshwa kwa kutengewa rasilimali ya kipato cha Ugatuzi na katika Hazina ya Usawa wa Mgao.

Utendakazi wa Kiugatuzi wa Kaunti utagharimu shilingi bilioni 148 katika mwaka wa 2012/13 (ikiwa ni 26% ya mapato yaliyokaguliwa). Katika kipindi cha kubadilisha mamlaka, Serikali Kuu itaendelea kutoa Huduma hizo mpaka kipindi ambacho kaunti zitakapokuwa na uwezo wa kujisimamia zenyewe.

Shilingi bilioni 5.5 zimetengewa Hazina ya Usawa wa Migao kwa kipindi cha miaka miwili ya kifedha 2011/12 na 2012/13. Mgao huo wa 2011/12 wa shilingi bilioni 2.5 utatumiwa kwa maji, barabara, shughuli za kiafya na umeme kama inavyoelekeza Katiba, huku shilingi bilioni 3.0 za mwaka wa 2012/13 zikisubiria kuamuliwa na kuchapishwa kwa vigezo vya jinsi ya kutambua maeneo halisi ya kugawiwa ngawira hiyo na Tume ya Ugawaji wa Mapato (CRA).

## UIMARISHAJI WA MAZINGIRA YETU YA KIBIASHARA ILI KUVUTIA UWEKEZAJI


Bajeti ya mwaka wa 2012/13 itaendelea kuongezea uwekezaki wa umma kwenye miundombinu ya sekta za Barabara, Kawi, Reli na Bandari ili kushughulikia nakisi ya muundombinsi wetu na kuwarahisishia wawekezaji kufanya kazi hapa nchini Kenya. .Shilingi bilioni 267.3 zimetengewa muundomsingi wa maendeleo ikilinganishwa na shilingi bilioni 221.4 zilizokuwa zimewekezwa katika mwaka wa 2011/12, ikiwasilisha ukuwaji wa 20.7 % . Hususan, sekta ya barabara ilitengewa shilingi bilioni 123.6, kawi (shilingi bilioni 79.9), Sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT) ( shilingi bilioni 7.2 ) kati ya wengine.

Katika ngazi ya usimamizi, mabadiliko ya Mahakama, Mabadiliko ya Huduma za sera na kuandaa mifumo ya usimamizi wa Bunge la Kitaifa katika ngazi ya Kaunti imeshughulikiwa kikamilifu na bajeti hii. Ubadilishanaji wa mamlaka katika mifumo ya ugatuzi baada ya uchaguzi Mkuu ujao unatazamiwa kuimarisha viwango vyetu vya ufanyaji biashara katika kaunti zitakazovutia wawekezaji.

Masjala ya Afisi ya Ardhi katika mfumo wa kidijitali unatazamiwa utapunguza matatizo ya utafutaji wa nyaraka na stakabadhi za ardhi na kufuatia hali hiyo itapunguza athari za kiwango cha juu cha bima kinachotozwa. Tayari maandalizi yamekamilika na kinachosubiriwa ni utekelezwaji tu katika mwaka wa 2012/13.

Katika Marekebisho ya Polisi, rasilimali za kutosha zimetengewa Kikosi cha Polisi cha Kenya ili kuhakikisha kwamba Usalama wa Ndani na ufuataji wa sheria unazingatiwa, hasa katika harakati za uchaguzi mkuu ujao. Hazina hizo pia zitasaidia katika utekelezwaji wa marekebisho yanayohitajika kama ilivyo katika katiba Mpya, ikiwa ni pamoja na kuajiri polisi wengine katika kikosi.

Kadhalika kupunguza tishio la kutoka nje ya mipaka ya nchi kwa usalama wetu wa kitaifa na pia kuimarisha biashara za humu nchini na hali kadhalika katika eneo la Afrika Mashariki, mgao wa bajeti uliotengewa Ulinzi na Ujasusi wa Kitaifa umeongezwa na kufikia shilingi bilioni 83.5 ikilinganishwa na shilingi bilioni 78 zilizokuwa zimetengwa katika mwaka wa 2011/12.



# ABBREVIATIONS

| | |
|---|---|
| CCF | Civil Contingency Fund |
| CDF | Constituency Development Fund |
| CFS | Consolidated Fund Services, includes Public debt Service, Pensions |
| ECD | Early Childhood Development |
| ESP | Economic Stimulus Programme |
| FDSE | Free Day Secondary Education |
| GECLA | General Economic, Commercial & Labour Affairs |
| GJLOS | Governance, Justice, Law and Order Sector |
| HM | Home Affairs |
| ICT | Information Communication Technology |
| IEBC | Independent Electoral & Boundaries Commission |
| KKV | Kazi Kwa Vijana |
| LATF | Local Authorities Transfer Fund |
| MOF | Ministry of Finance |
| NSIS | National Security Intelligence Service |
| OVC | Orphans and Vulnerable Children |
| SGR | Strategic Grain Reserve |

**MUHIMU:**

- *Si lazima kwa hesabu hizi kuwa jumla kamili kutokana na ukadiriaji wa:*
- *Kwa ESP, KKV na KYEP, hazina hizi zimesambazwa kwenye sekta mbali mbali;*
- *Rejelea makadirio ya kina katika wizara mbali mbali;*
- *Rangi ya kijivu: Jumla ya bajeti ya Taifa ikiwemo Idara ya Mahakama na Bunge;*
- *Rangi ya chungwa: Matumizi katika sekta muhimu:*
- *Sehemu ya chini ya jedwali, matumizi kwa ukuaji huku sehemu nyingine ikiwakilisha matumizi mabaya.*
- *Jedwali hazijachorwa kwa kipimo.*

MINISTRY OF FINANCE
TREASURY BUILDING, HARAMBEE AVENUE
P.O. Box 30007 - 00100, Nairobi-Kenya • Tel: +254 (0)20 2252299, 0733 660606 / 0728 338111
Email: profinance@treasury.go.ke • Website: www.treasury.go.ke

*Matumizi bora ya Fedha wajibu wetu*